

## **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI (PRESS RELEASE)**

Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limelazimika kusitisha rasmi shughuli za uzalishaji (Prohibitory Notice) katika kiwanda cha METRO STEEL MILL kilichoko Kipawa, Dar Es Salaam kuanzia leo. Hatua hiyo imechukuliwa baada ya Uongozi wa kampuni hiyo kukiuka na kushindwa kutekeleza ushauri na maagizo halali waliyopewa ili kupunguza tatizo la moshi mzito unaosababishwa na shughuli za uzalishaji wa chuma katika kiwanda hicho kwa kutumia mali ghafi ya vyuma chakavu. Hatua hii iliyochukuliwa na Baraza ni utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ambayo imepitishwa na Bunge Novemba, 2004 na imeanza kufanya kazi rasmi mwezi Julai 2005.

Kiwanda cha Metro Steel Mills kilichopo eneo la Kipawa barabara ya Nyerere kinatengeneza nondo. Shughuli za uzalishaji wa Kiwanda cha Metro Steel Mills zimelalamikiwa na wakazi wa maeneo hayo kuwa zinasababisha athari kubwa kwa afya zao na uchafuzi wa mazingira. Baadhi ya matatizo makuu yaliyobainika katika kiwanda hicho ni ujenzi mbaya wa mtambo, kukosekana kwa mfumo madhubuti wa kutolea moshi mzito utokanao na uzalishaji wa nondo, usafi hafifu ndani ya kiwanda ambao unahatarisha maisha ya wafanyakazi kwa kutotumia vitendea kazi bora kama vile vichuja hewa vya pua na midomo. Moshi mzito unasababisha kero kubwa kwa wakazi wanaozunguka kiwanda hicho tangu kiwanda kiliposajiliwa mwaka 2003.

Baraza ilipokea barua ya malalamiko ya kwanza Mwezi April 2004 toka kampuni ya Stanley Mining (ambao walikuwa wapangaji jirani) na pia Mh. Waziri wa Nchi (Mazingira) aliandikiwa barua na waathirika na hivyo aliliagiza Baraza kushughulikia tatizo hilo haraka iwezekanavyo. Baraza lilitembelea na kufanya ukaguzi na kuushauri uongozi wa kiwanda kuchukua hatua za haraka ili kupunguza athari hizo. Mwezi Machi 2005 Baraza lilifanya mkutano wa wadau (Manispaa ya Ilala na Jiji) kuhusu tatizo hili na walitembelea kiwanda hicho. Wadau walitoa maelekezo ya pamoja kwa kampuni ili kurekebisha matatizo hayo katika kipindi kisichozidi miezi minne kuanzia Mei 2005. Mwekezaji hakuonyesha ushirikiano na kutokana na utekelezaji hafifu, Mwezi Juni 2005 Baraza lilitoa onyo kali kwa Kampuni hiyo na kuwataka kusitisha shughuli za uzalishaji mpaka pale watakaporekebisha mfumo wa uzalishaji. Kwani kuendeleza uzalishaji